SUMAIT University Journal (SUJ)
eissn (2953-2698)
Issue No.18 June 2026

# MSUKUMO WA UVAAJI WA UHUSIKA WA KIKE KWA WAIGIZAJI WA KIUME KATIKA KOMEDIA ZA KISWAHILI NCHINI TANZANIA

Khadija Khamis Moh'd (khadijakhamism@gmail.com)
Dkt. Zainab Ali Iddi (zainab.iddi@suza.ac.tz)
Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar

*Received: October 2025, accepted: Juanuray 2026 Published: June 2026*
*© SUMAIT University Journal 2026*

## Abstract
*The main purpose of this article is to examine the factors that motivate male actors to portray female charactors in Swahili comedies in Tanzania. This investigation was guided by the Reception Theor. The study was conducted in the Urban West Region on Unguja Island. A total of 20 informants were participated, including elders, youths, students and performers from a special acting troupe. Data collected through interviews and analysed using a descriptive approach. Findings have revealed that seeking income, empowerment, entertainment, and others have been discovered. Overall, this study contributed new knowledge by highlighting the reasons behind such portrayals from the community's perspevtives and uncovering how gender concepts are constructed, reflected and received in artistic works, especially comedy.`*

## 1.0 Utangulizi
### 1.1 Fasili ya Istilahi na Dhana Muhimu
Sehemu hii inatoa fasili na ufafanuzi wa istilahi na dhana muhimu zilizotumika katika utafiti huu. Fasili na ufafanuzi huo umetolewa ili kusaidia kuelewa kwa uwazi zaidi. Istilahi na dhana hizo ni kama zifuatavyo:

1.1.1 Komedia: ni tamthilia fupi ya kuchekesha inayowasilishwa kupitia mitandao au majukwaa ya sanaa kwa madhumuni ya kuburudisha na kufikisha ujumbe kwa jamii.

1.1.2 Uhusika: ni mtindo wa kuwasawiri wahusika kupitia mavazi, lugha, matendo na mitazamo yao kwa lengo la kuwasilisha ujumbe fulani katika komedia.

1.1.3 Uvaaji wa Uhusika wa kike: Mohamed (1995) anaeleza kuwa uvaaji wa uhusika ni mbinu ya kisanaa inayomwezesha mchekeshaji kubadilika kimuonekano ili kuwakilisha taswira tafauti za kijamii. Kwa mujibu wa utafiti huu, uvaaji wa uhusika ni hali ya waigizaji wa kiume kuvaa mavazi na tabia za kike kwa madhumuni ya kufikisha ujumbe wa burudani au kijamii katika komedia.

1.1.4 Jinsia: Butler (1990) anafasili jinsia kuwa ni ujenzi wa kijamii unaozingatia tafauti za kijinsia katika matamshi, tabia na nafasi za kijamii. Kwa mujibu wa utafiti huu, jinsia inahusu muktadha wa kijamii unaotafautisha uhusika wa kike na wa kiume katika maigizo, siyo tu kwa misingi ya kibaolojia bali pia kwa tabia na mitazamo.

1.1.5 Wahusika: ni waigizaji katika komedia wanaobeba ujumbe kwa kutumia taswira mbalimbali, ikiwemo ya jinsia tafauti na ile waliyo nayo kiasili.

1.1.6 Utambulisho wa Kisanaa: unahusu namna msanii wa komedia anavyotumia mavazi ya kike, lafudhi, ishara na mitindo ya kike ili kuwasilisha uhusika wa kipekee kwa hadhira. Mtindo huu wa kujitambulisha kisanaa hujenga muktadha wa kujadiliwa na jamii kuhusu nafasi ya sanaa, mipaka ya ubunifu na maadili ya kijamii.

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Komedia ni utanzu wa fasihi simulizi ambao huwasilisha matukio ya kufikirika au halisi kwa njia ya kuchekesha, huku lengo lake kuu likiwa ni kuburudisha, kuelimisha na wakati mwengine kuibua hoja za kijamii kwa namna ya kejeli au mzaha. Kwa mujibu wa Kennedy na Gioia (2007), komedia ni sanaa inayolenga kuonesha mapungufu ya kijamii, kitabia au kimfumo kwa njia ya kuchekesha na kumfanya mtazamaji au msomaji atafakari hali halisi ya maisha yake. Asili ya komedia inatokana na neno la Kigiriki "comos" likimaanisha sherehe za kijamii zilizokuwa zinaambatana na ngoma, vicheko, majigambo na uimbaji, kwa ajili ya kumheshimu mungu Dionysius, mungu wa rutuba na mavuno kwa Wayunani wa kale.

Katika karne ya 18 na 19, wachekeshaji mashuhuri kama Charlie Chaplin na Stan Laurel waliendeleza dhana ya komedia kwa kuibua mitindo mipya ya maigizo ya kuchekesha kupitia filamu na michezo ya kuigiza. Chaplin na Laurel walijulikana kwa kuuvaa uhusika wa kike katika baadhi ya filamu zao, jambo ambalo liliwavutia watazamaji kwa sababu ya ucheshi wake, lakini pia lilizua mijadala kuhusu tafsiri ya kijinsia katika sanaa ya uigizaji (Decherney, 2011). Uvaaji huu wa uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume ulitokana na mtindo wa vichekesho vya jukwaani, ambapo mavazi na matendo vilitumika kama mbinu ya kuamsha hisia na kupeleka ujumbe kwa hadhira.

Hali hii iliendelea hadi kufikia bara la Afrika ikiwemo nchi ya Tanzania, ambapo kulingana na Mulokozi (2017), aina za komedia zilianza kushamiri tangu miaka ya 1920 kwa madhumuni ya kuburudisha na kuelimisha jamii kupitia vituko vya kuchekesha. Tangu wakati huo, sanaa ya vichekesho imeendelea kukua, huku wachekeshaji wa makundi mbalimbali wakijitokeza, bila kujali jinsia, rika au hali zao za kiafya. Katika kipindi cha karne ya 21, kuanzia miaka ya 2000, kumekuwepo na ongezeko kubwa la wachekeshaji wanaotumia mitandao ya kijamii, televisheni na majukwaa mengine ya mawasiliano kuwasilisha kazi zao, ikiwemo matumizi ya uvaaji wa uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume.

Uhusika katika fasihi hujumuisha mbinu na mikakati ya kisanaa inayotumiwa na waandishi au waigizaji kuonesha maisha ya muhusika, ikiwemo matendo, lugha, mavazi, tabia na muktadha wa kijamii (Abrahams, 1992). Uvaaji wa uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume unarejelea hali ambayo mwanamme huigiza au kujimithilisha kama mwanamke kwa kuvaa mavazi ya kike, kutumia mitindo ya lugha ya wanawake na kuiga tabia zao kwa madhumuni ya kuibua kicheko au kufikisha ujumbe kwa hadhira. Mohamed (1995) anaeleza kuwa hii ni mbinu mahususi ya kisanaa inayoweza kuibua hisia za kicheko, hasa inapohusisha utafauti wa kijinsia katika mazingira ya kawaida ya kijamii.

Hata hivyo, licha ya kukubalika kwa kiwango fulani katika jamii, mtindo huu wa waigizaji wa kiume kuvaa uhusika wa kike umeendelea kuzua mijadala kuhusu tafsiri zake kijamii, kimaadili na kiutamaduni. Kwa mujibu wa Bakhtin (1984), komedia huweza kuwa uwanja wa ‘mijadala ya sauti nyingi’ ambapo mitazamo kinzani ya kijamii huibuka na kuchochea tafakuri. Muktadha wa Tanzania, ambao umejengwa katika misingi ya mila, desturi na maadili ya Kiafrika na Kiislamu au Kikristo, huenda ukapokea dhana hii kwa mitazamo tafauti.

Hii ndiyo sababu ya msingi iliyomsukuma mtafiti kufanya utafiti huu, kwani licha ya ongezeko la matumizi ya mbinu hii katika komedia, bado mtafiti hajaona utafiti unaochambua dhana ya uvaaji wa uhusika wa kike na waigizaji wa kiume kwa mtazamo wa kisanaa, kijamii na kiutamaduni. Hivyo basi, utafiti huu ulichunguza kwa undani jambo hili, ili kuchangia katika hazina ya maarifa ya fasihi na kutoa mwelekeo wa kitaalamu kuhusu nafasi ya mbinu hii katika jamii ya Kiswahili.

## 2.0 Tatizo la Utafiti

Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na ongezeko la wachekeshaji wa Kiswahili, hususan kupitia mitandao ya kijamii kama TikTok na YouTube, ambao huvaa na kuwasilisha uhusika wa kike huku wao wakiwa waigizaji wa kiume. Mtindo huu umeibua mjadala mpana miongoni mwa wanajamii kuhusu maadili, taswira ya jinsia, burudani na nafasi ya sanaa ya uigizaji katika jamii ya Kitanzania. Ingawa uvaaji huu wa uhusika wa kike unaonekana kuwa wa kawaida na wa kuvutia kwa baadhi ya watazamaji, bado sababu mahususi zinazowasukuma waigizaji wa kiume kuwasilisha uhusika huo hazijaelezwa katika tafiti zilizopo na hazijafanyiwa uchambuzi wa kitaalamu. Hivyo basi, utafiti huu unalenga kuchunguza uvaaji wa uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume katika komedia za Kiswahili, kwa kuangalia vichocheo vya kisanaa na kijamii pamoja na mapokezi ya hadhira kulingana na muktadha wa kiutamaduni.

## 3.0 Nadharia ya Utafiti

Nadharia ni nyenzo, mawazo, maelezo au muongozo mkuu uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua na kuelekeza jambo fulani (TUKI 2004). Mtafiti aliongozwa na Nadharia ya Upokezi wa Hadhira katika uchambuzi wake kama ifuatavyo:

### 3.1 Nadharia ya Upokezi wa Hadhira

Nadharia ya Upokezi wa Hadhira ni mkabala wa kifasihi na mawasiliano unaoangazia namna hadhira inavyopokea, kutafsiri na kuathiriwa na matini au ujumbe wa kifasihi na media. Nadharia hii inajikita katika dhana kwamba maana haibandikwi tu na mtunzi au mtayarishaji, bali huundwa upya na msomaji au mtazamaji kulingana na muktadha wake wa kijamii, kitamaduni na kihistoria.

Nadharia hii ni tanzu ya nadharia ya mwitiko wa msomaji ambayo iliasisiwa na wanafalsafa wa Kijerumani Hans Robert Jauss na Wolfgang Iser katika miaka ya 1960 kupitia Shule ya Constance, Ujerumani. Walisisitiza kuwa msomaji ana nafasi muhimu katika kuleta maana ya kazi ya kifasihi, kwa sababu kila msomaji huathiriwa na upeo wa matarajio yake unaotokana na maarifa, uzoefu na muktadha wake binafsi.

Mchango mkubwa zaidi katika kukuza nadharia hii ulitolewa na mwananadharia wa mawasiliano ya utamaduni, Stuart Hall (1973), kupitia insha yake alibainisha kuwa mawasiliano ya media

hayaleti maana moja kwa moja, bali hupitia hatua ya "usimbaji" na "usimbuaji", ambapo wasikilizaji au watazamaji wanaweza kupokea ujumbe kwa namna tatu: (i) kukubaliana na ujumbe, (ii) kuupokea kwa tahadhari au (iii) kuukataa kabisa.

Webster (1998) na Jin (2011) ni miongoni mwa wataalamu waliokuza zaidi nadharia hii kwa kuieleza katika mazingira mapana ya kijamii na kiutamaduni. Katika muktadha wa utafiti huu nadharia hii inasaidia kuchunguza namna hadhira ya Kiswahili inavyopokea na kutafsiri uvaaji wa uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume katika komedia. Data za utafiti zilichambuliwa kupitia msingi wa pili wa nadharia hii unaoeleza kuwa; Watazamaji wanaweza kutambua kuwa baadhi ya maudhui au vitendo vilivyowasilishwa si sahihi kijamii au kimaadili, lakini bado wakavikubali kwa kuelewa mantiki, dhamira au ujumbe uliofichika nyuma ya mawasilisho hayo; ambapo mtafiti aligundua sababu za uvaaji huo.

### 3.1.2 Mihimili ya Nadharia ya Upokezi wa Hadhira

Nadharia hii ina mihimili mikuu mitatu, ambayo hufafanuliwa kama ifuatavyo:

Kwanza: Hadhira huitafsiri kazi ya sanaa au mawasiliano ya media kwa kuzingatia historia yao binafsi ya kijamii, kiutamaduni na uzoefu wa maisha. Mtazamo wao hutegemea mazingira waliyokulia, imani walizo nazo na muktadha wao wa kijamii.

Pili: Watazamaji wanaweza kutambua kuwa baadhi ya maudhui au vitendo vilivyowasilishwa si sahihi kijamii au kimaadili, lakini bado wakavikubali au kuvisamehe kwa kuelewa mantiki, dhamira au ujumbe uliofichika nyuma ya mawasilisho hayo.

Tatu: Hadhira ni wakosoaji hai wa kazi za sanaa; hupokea na kutathmini kazi hizo kwa mitazamo tafauti na kutoa maoni yao kulingana na namna wanavyohusisha yaliyomo na hali halisi ya kijamii, kiutamaduni na kiitikadi katika maisha yao.

## 4.0 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Kothari (1990) anabainisha kuwa ukusanyaji wa data ni hatua ya awali na muhimu katika mchakato wa utafiti, inayomuwezesha mtafiti kupata taarifa mahsusi zitakazomsaidia kufikia malengo ya utafiti wake. Mbinu za ukusanyaji wa data ndizo nguzo kuu za kupata taarifa sahihi, zinazojibu maswali ya utafiti. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu ya usaili, ambapo aliwauliza maswali watoataarifa wake ambao ni waigizaji (JKU), wanafunzi wa fasihi, wazee na vijana aliowateua. Mtafiti alitumia mbinu hii ili kupata data za msingi, yaani taarifa zilizokusanywa kwa mara ya kwanza moja kwa moja kutoka uwanjani (Moyles, 2002). Aliteua jumla ya maswali 5 ya wazi, mafupi na yanayofahamika kirahisi na kurekodiwa. Maswali hayo yaliwasilishwa kwa makundi teule ya watoataarifa na majibu yalirekodiwa kwa kutumia simu ya kiganjani. Mwongozo wa usaili ulimsaidia mtafiti kuendesha usaili huo kwa utaratibu, kuhakikisha masuala yote muhimu yanajadiliwa na kupunguza uwezekano wa kupoteza mwelekeo wakati wa usaili.

Baadaye, majibu hayo yalihaririwa na kuchambuliwa kwa uangalifu mkubwa ili kupata muktadha sahihi wa sababu zinazowasukuma waigizaji wa kiume kuuvaa uhusika wa kike. Mbinu hii ilimuwezesha mtafiti kupata maelezo, yaliyojaa hoja, mitazamo na hisia halisi za walengwa, hivyo kuimarisha uhalali na usahihi wa data zilizokusanywa.

Mtafiti alitumia mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo ili kuchambua data zilizokusanywa kutoka kwa watoataarifa. Mkabala huu wa kimaelezo hutumika katika tafiti zinazolenga kueleza na kufafanua maana ya matukio au mitazamo ya watu, kwa kutumia maneno badala ya takwimu. Mtafiti alikusudia kuelewa kwa undani sababu zinazohusu uvaaji wa uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume katika komedia za Kiswahili, hivyo uchambuzi huu ulilenga kuibua maana zilizojificha kwenye kauli, matendo na mitazamo ya watoataarifa.

## 5.0 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kuna sababu mbalimbali zinazopelekea waigizaji wa kiume kuvaa uhusika wa kike, zikiwemo sababu za kisanaa, kijamii, kiutendaji na kibiashara. Sababu hizi zimeelezwa na watoataarifa kutoka makundi tafauti kama wanafunzi, waigizaji, wazee na vijana.

### 5.1 Sababu za Waigizaji wa Kiume Kuvaa Uhusika wa Kike

Katika sehemu hii, mtafiti anawasilisha data zinazolenga kuchunguza sababu za waigizaji wa kiume kuvaa uhusika wa kike katika komedia za Kiswahili. Data hizi zilipatikana kwa kutumia mbinu ya usaili na watoataarifa walioteuliwa. Data zilichambuliwa kwa kuhusisha na mhimili wa pili wa nadharia ya Upokezi wa Hadhira unaosema kuwa; Watazamaji wanaweza kutambua kuwa baadhi ya maudhui au vitendo vilivyowasilishwa si sahihi kijamii au kimaadili, lakini bado wakavikubali au kuvisamehe kwa kuelewa mantiki, dhamira au ujumbe uliofichika nyuma ya mawasilisho hayo.
Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kuna sababu mbalimbali zinazosababisha waigizaji wa kiume kuvaa uhusika wa kike, zikiwemo sababu za kisanaa, kijamii, kiutendaji na kibiashara. Sababu hizi zimeelezwa na watoataarifa kutoka makundi tafauti kama wanafunzi, waigizaji, wazee na vijana kama ifuatavyo:

#### 5.1.1 Kutafuta Kipato

Katika uchambuzi wa uvaaji wa uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume katika komedia za Kiswahili, imebainika kuwa mojawapo ya sababu kuu ni kutafuta kipato. Waigizaji hutumia mbinu na mitindo mbalimbali katika kazi zao za sanaa ili kuwavutia watazamaji na hatimaye kujipatia kipato.

Baadhi ya watoataarifa walieleza kuwa:

"*Wasanii wapo wengi na kila mmoja anafikiria kitu gani afanye ili aweze kutoka kimaisha kutoka sehemu moja kwenda nyengine na wakati mwengine anaweza kulifanya jambo ambalo halipo katika damu yake, lakini anafanya ili mkono uwende kinywani*".

Chanzo: Data ya Uwandani (2025)

Kauli hii inasisitiza kuwa msanii anaweza kuchagua mtindo wowote utakaomuwezesha kujikwamua kiuchumi, hata kama hauendani na mielekeo ya awali ya sanaa yake. Katika muktadha huu, kuvaa uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume kunaonekana kuwa mbinu mojawapo inayoongeza mvuto wa komedia na kuvutia watazamaji wengi zaidi. Hii inaonekana dhahiri kwa mfano wa Joti, ambaye kufikia mwaka 2024 alikuwa ana zaidi ya wafuasi milioni tatu na laki nne katika mtandao wa YouTube, ukilinganisha na Pungasese aliyekuwa na wafuasi laki mbili na elfu

arobaini na mbili. Tafauti hii ya ushawishi inaonesha kuwa mbinu ya uigizaji inayojumuisha uhusika wa kike inaweza kuongeza mapato kupitia majukwaa ya kidijitali.

Watoataarifa wengine waliongeza:

"*Msanii yeyote anapobuni kazi yake na kuiwasilisha kwa jamii kwa njia yoyote ile anayoipenda na ikakubalika, msanii huyo ni mwenye kufanikiwa, wasanii mbalimbali wa komedia wanauvaa uhusika wa kike ili kujiengezea kipato".*

Chanzo: Data ya Uwandani (2025)

Kwa mujibu wa nadharia ya Hall (1973), watazamaji wanaweza kutambua baadhi ya maudhui au vitendo vinavyowasilishwa si sahihi kijamii au kimaadili, lakini bado wanavikubali kutokana na dhamira au ujumbe uliofichika nyuma yake. Katika muktadha huu, uvaaji wa uhusika wa kike ni tendo la kijamii linalotimiza jukumu la kiuchumi kupitia lugha ya vitendo vya sanaa.

Vilevile, Lucas na Seleman (2022) wanaeleza kuwa kazi ya sanaa huweza kubeba ujumbe au athari ya kijamii ikiwa msanii atautumia utendaji wake kwa umahiri ili kuwagusa walengwa. Aidha, Njogu (2010) anathibitisha kuwa sanaa ya uigizaji inaweza kutumika kama kitega uchumi iwapo itabuniwa kwa kuzingatia mahitaji na mabadiliko ya kijamii. Kwa hivyo, uvaaji wa uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume si tu mbinu ya kisanaa, bali pia ni mkakati wa kiuchumi unaochochewa na mazingira ya soko la burudani.

Hii inaonesha kuwa, kwa kutumia mitindo ya uigizaji wa jinsia tafauti, waigizaji wanatengeneza nafasi mpya za kipato huku wakikidhi matarajio ya hadhira yao.

### 5.1.2 Ubunifu Mpya

Ubunifu ni uwezo wa mtu kuunda, kubadilisha au kubuni jambo jipya lenye mvuto na maana katika jamii. Kwa mujibu wa Ndalu, Babusa na Mirikau (2014), ubunifu ni hali ya kufikiria na kuunda kitu au jambo kwa njia ya kipekee inayovuka mipaka ya kawaida ya fikra au mazoea ya jamii. Katika muktadha wa uigizaji wa komedia za Kiswahili, ubunifu una nafasi muhimu katika kuwafanya wasanii wajitafautishe na wenzao kwa kutumia mitindo mipya isiyozoeleka.

Utafiti huu umebaini kuwa, waigizaji wanaovaa uhusika wa kike wanatumia njia hii kama mbinu ya ubunifu wa kisanaa inayotumika kuvunja mazoea ya uigizaji wa kijinsia wa moja kwa moja. Hill (1977) anasema kuwa usawiri bora wa wahusika huhitaji hali ya juu ya ubunifu ili kuwafanya wahusika hao wadhihirishe hali halisi zinazojitokeza katika jamii.

Kauli hii inaungwa mkono na mtoataarifa J ambaye alisema:

"*Wakati mwengine, baadhi ya wasanii hubuni vitu vilivyo tafauti na jamii zetu au kuigiza vitu ambavyo vilibuniwa na watu wa mataifa mbalimbali, wao wanaonekana kuvileta katika jamii zetu na kuviboresha*".

Chanzo: Data ya Uwandani (2025)

Muktadha huu unaonesha kuwa ubunifu si lazima utokane na mazingira ya ndani pekee bali unaweza kuchochewa na muktadha wa kimataifa. Waigizaji wanautumia mtindo wa kuvaa uhusika wa kike kama njia ya kuleta ubunifu mpya, si kwa lengo la kuiga tu, bali kuutafsiri na kuurekebisha kwa mujibu wa mazingira ya jamii zao.

Ingawa mtafiti ameshaeleza kuwa, uvaaji huu wa uhusika wa kike ulianzia zamani duniani, lakini upya wake umekuja katika jamii yetu kwamba, uvaaji huu umekuja kubadili mazoea ya hali halisi ya tasnia ya maigizo yetu katika komedia, kutokana na mazingira ya sanaa na tamaduni zetu. Hivyo basi, ubunifu huu unabadili uhalisia na kuchokoza fikra za wanajamii kuhusiana na ujumbe unaopelekwa kwa hadhira.

Kwa mujibu wa nadharia ya upokezi wa hadhira (Hall 1973), mitindo ya kisanaa hutegemea sababu zilizofichwa katika uwasilishaji wa maudhui. Uvaaji wa uhusika wa kike unaakisi lengo la msanii kujenga upya uhalisia wa kijamii na kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kisanii. Hii ni kwa sababu msanii hutumia sanaa yake kama jukwaa la kueleza, kushirikisha na kuhamasisha jamii kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

Lucas na Seleman (2022) wanaeleza kuwa, kazi za sanaa hujitokeza kwa njia za ubunifu na ubunifu huo ndio unaotoa upekee wa kazi hiyo mbele ya hadhira. Hii inaendana na hoja ya Wamitila (2002) kwamba ubunifu wa kifasihi hujikita katika uwezo wa msanii kubadili au kuumba upya uhalisia ili kuwagusa walengwa.

Kwa hiyo, uvaaji wa uhusika wa kike unaonekana kama mbinu ya kisanaa iliyojaa ubunifu mpya unaolenga kuchokoza fikra, kufikisha ujumbe na kupanua mawanda ya fasihi ya Kiswahili ya kisasa.

**5.1.3 Ubinafsi**

Ubinafsi ni tabia ya mtu kujihusisha mno na masilahi binafsi huku akipuuza au kutojali mahitaji na fursa za wengine. Albrecht (2012) anaeleza ubinafsi kama hali ya mtu kujipendelea kupita kiasi, kushindwa kushirikiana na kutotegemea au kusaidia wengine hata wanapohitaji msaada. Katika muktadha wa komedia za Kiswahili, utafiti huu umebaini kuwa ubinafsi ni mojawapo ya sababu zinazochochea waigizaji wa kiume kuvaa uhusika wa kike badala ya kuwawezesha wanawake wenyewe kuigiza nafasi hizo. Baadhi ya watoa taarifa wamelalamikia mwenendo huu, wakiona kuwa unawanyima fursa wanawake kuonesha vipaji vyao vya kisanaa. Mmoja alisema:

"*Kufanya hivyo kunampelekea msanii kuonekana ana uchoyo wa nafsi... baadhi ya wanawake wanavipaji ila hawana wa kuwashika mkono... wanaweza kufanya kazi nzuri kuliko hata wanaume".*

Chanzo: Data ya Uwandani (2025)

Uchambuzi wa data unaonesha kuwa waigizaji kama Joti na Pungasese mara nyingi huigiza nafasi nyingi katika komedia moja, wakiwa baba, mtoto, babu au mwanamke. Hili linaweza kutafsiriwa kama dalili ya ubinafsi wa kisanii, ambapo nafasi zinazoweza kupewa wasanii wengine, hasa wanawake, hutwaliwa na mtu mmoja kwa lengo la kujiinua mwenyewe kisanaa. Hali hii inatokana na ukosefu wa fursa au msaada kwa wanawake, jambo linalozuia kukuza vipaji vipya.

Kwa mujibu wa Hall (1973), mazungumzo yanayosomwa na watazamaji ambao wanafahamu vitendo vilivyofanywa kwenye maigizo hayo si sahihi, lakini waendelee kukubali kuwa ni sawa kwa kuwa kuna sababu nyuma yake zilizofichwa. Hali ya wanaume kuvaa uhusika wa kike huweza kuakisi muktadha wa ukosefu wa usawa wa kijinsia katika fursa za kisanaa. Nadharia hii husaidia kuelewa kuwa mtindo huu wa uwasilishaji wa maudhui hupelekea hadhira kukubali au kukataa mitindo hiyo kulingana na mahusiano ya kijamii yaliyopo katika jamii husika.

Kwa upande wa kijinsia, Limbe (2014) anaeleza kuwa wasanii wanawake hawapewi nafasi ya kuwasilisha uhuru wao wa kisanaa kwa kiwango sawa na wanaume na mara nyingi hutiliwa shaka pindi wanapojaribu kuwakejeli wanaume kama sehemu ya sanaa yao. Aidha, Romos, Costa na Cerqueira-Santos (2020) wanaonesha kuwa sanaa inaweza kuathiriwa sana na mielekeo ya kijamii na mitazamo ya kijinsia, jambo linalowafanya baadhi ya wanawake kushindwa kushiriki kikamilifu katika sekta ya burudani.

Kwa hivyo, uvaaji wa uhusika wa kike na waigizaji wa kiume unaelezwa kama mbinu ya kisanii na pia kama kielelezo cha ubinafsi na ukosefu wa ushirikishwaji wa kijinsia katika komedia za Kiswahili, hali inayozua mjadala kuhusu usawa wa kijinsia katika uwanja wa sanaa.

**5.1.4 Uwezeshwaji**

Katika utafiti huu, uwezeshwaji umetambuliwa kama mojawapo ya sababu kuu zinazochochea waigizaji wa kiume kuvaa uhusika wa kike katika komedia za Kiswahili. Kwa mujibu wa Ndalu, Babusa na Mirikau (2014), uwezeshwaji ni hali ya kumpa mtu rasilimali, msaada au mazingira rafiki ili aweze kufikia malengo yake.

Katika muktadha wa komedia, baadhi ya waigizaji wanaonekana kupewa fursa na uungwaji mkono wa kifedha, kijamii au kimfumo, hali inayowawezesha kutumia mtindo huu kwa kujiamini na kwa mwendelezo wa kazi zao. Baadhi ya watoataarifa walieleza kuwa:

*"Waigizaji wanadhaminiwa na mtu au kikundi cha watu kwa malengo maalumu nao hutumia mtindo huu kwa kujiamini kwa sababu kuna watu ambao wanaweza kuwalinda au kuwatetea pamoja na kuziboresha kazi zao".*

Chanzo: Data ya Uwandani (2025)

Hali hii inajidhihirisha pia katika matumizi ya uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume katika matangazo ya kibiashara kama vile bidhaa za watoto, vipodozi, vifaa vya ujenzi au huduma mbalimbali, ambapo waigizaji hao huvutia hisia na kuaminika zaidi kwa hadhira kutokana na mtindo wao wa kipekee wa uwasilishaji.

Mtoataarifa B aliongeza:

"*Waigizaji wanarubuniwa ili kuigiza nafasi za wanawake na kurubuniwa huko si lazima wapewe pesa lakini hata kupewa sifa tu na watu wengine".*

Chanzo: Data ya Uwandani (2025)

Kwa mujibu wa Frankelius (2009), uwezeshwaji wa wabunifu unahitaji mazingira ya kuwaamini, kuwathamini na kuwawezesha kwa kuwapatia elimu, mitaji na ulinzi wa kazi zao. Uwekezaji huu huongeza ubunifu na utendaji bora katika sanaa.

Kwa kuhusisha na Hall (1973), watazamaji wanaweza kutambua kuwa baadhi ya maudhui na vitendo vinavyowasilishwa si sahihi kijamii na kimaadili, lakini wakavikubali kutokana sababu zilizofichikana nyuma yake. Katika muktadha huu, mtindo wa uvaaji wa uhusika wa kike unaungwa mkono na mazingira yanayowawezesha wasanii kutumia lugha, utendaji na mavazi ya kike kama njia ya kufikisha ujumbe, kujitambulisha na kuongeza ushawishi wao katika jamii.

Pia, Lucas na Seleman (2022) wanaeleza kuwa mazingira chanya ya usanii huwezesha msanii kujieleza kikamilifu na kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa ili kutimiza madhumuni ya kazi yake.

Hivyo, utafiti huu umetambua kuwa uwezeshwaji una mchango mkubwa katika kuendeleza mtindo wa uvaaji wa uhusika wa kike, si tu kama burudani bali kama mbinu ya kufanikisha kazi za sanaa na kuwasilisha ujumbe unaolenga kuamsha fikra za kijamii.

**5.1.5 Kupata Umaarufu**

Umaarufu ni hali ya kutambulika au kuwa mashuhuri kwa kufanya jambo au shughuli fulani kwa ubingwa (TUKI, 2014). Utafiti huu umebaini kuwa mojawapo ya sababu za waigizaji wa kiume kuvaa uhusika wa kike katika komedia za Kiswahili ni hamu ya kutafuta umaarufu. Umaarufu huu hujengwa kupitia uwasilishaji wa kazi zenye mvuto, upekee na ubunifu wa hali ya juu.

Muigizaji Joti ni mfano halisi wa hali hii. Kulingana na Kamusi Elezo Huru (2024), Joti alianza kazi yake ya uchekeshaji kupitia kundi la Ensemble lililokuwa likirushwa na ITV, lakini hakupata umaarufu mkubwa. Umaarufu wake ulianza kuimarika baada ya kuanzisha kundi jipya la The Comedy kupitia EATV, ambapo alibadilika na kuanza kuvaa uhusika wa jinsia mbalimbali, hasa wa kike. Mbinu hii ilimjengea jina ndani na nje ya nchi na kumtafautisha na waigizaji wengine waliokuwa wakitumia mitindo iliyozoweleka. Kwa mujibu wa mmoja wa watoataarifa alieleza:

*"Wasanii wapo wengi mno nchini kwetu, lakini changamoto inayowakabili hawapati umaarufu kutokana na mitindo yao wanayoitumia ni hiyohiyo iliyozoweleka kila siku katika jamii. Ili watoboe, watafute mitindo mipya itakayowafanya wao kujuulikana zaidi na kusogeza mbele komedia zao".*

Chanzo: Data ya Uwandani (2025)

Kauli hii inaashiria kwamba uvaaji wa uhusika wa kike ni mbinu ya kujitafautisha kisanaa ili kuvutia hadhira na kupata umaarufu zaidi. Kwa kuhusisha na nadharia ya upokezi wa hadhira ya Stuart Hall (1973) tunaelewa kuwa watazamaji wanaweza kutambua kuwa baadhi ya maudhui au vitendo vinavyowasilishwa si sahihi kimaudhui na kimaadili, lakini bado wakavikubali kwa kuelewa mantiki, dhamira au ujumbe uliofichika katika mawasiliano hayo. Uvaaji wa uhusika wa kike katika komedia hizi unaonesha kuwa mtindo huu wa kutumia lugha, mavazi na utendaji unatumiwa kwa lengo la kujenga utambulisho mpya wa kisanaa na kuvutia jamii.

Kwa kuongezea, katika sanaa ya maonesho, umaarufu wa msanii hujengwa kupitia mtindo wa uwasilishaji unaobeba ubunifu, uigaji wa hali ya juu na uhalisia wa kijamii. Hivyo, waigizaji kama Joti na Pungasese wamefanikiwa kutumia mtindo huu kama nyenzo ya kujitangaza na kupata umaarufu mkubwa kwa kutumia uhusika wa kike kama kivutio cha kisanii.

**5.1.6 Kuburudisha**

Burudani ni kipengele muhimu katika kazi za fasihi kinachowekwa makusudi ili kuifurahisha na kuiburudisha hadhira. Katika muktadha wa uigizaji wa komedia za Kiswahili, miongoni mwa sababu kuu zinazowafanya waigizaji wa kiume kuvaa uhusika wa kike ni kuleta burudani kwa jamii. Uvaaji huu wa uhusika wa kike hujengwa katika msingi wa kuibua ucheshi, mshangao au ukinzani wa kijinsia unaochangamsha hadhira. Sambamba na hayo, kazi yoyote ya fasihi ikiwemo komedia inabakia kuwa ni sehemu ya burudani, hata bila ya kuwa na mtindo huu wa uvaaji wa uhusika wa kike, lakini bado pamoja na jambo hilo, kuna baadhi ya watu wanavutika zaidi na jambo hili ingawa fasihi yenyewe miongoni mwa dhima zake kuu ni kuburudisha.

Kwa mujibu wa Senkoro (2011), komedia ni kazi za kifasihi zilizo kinyume na tanzia, ambapo ucheshi wake hujengwa tangu mwanzo hadi mwisho wa kazi kwa lengo la kuiburudisha jamii kupitia matumizi ya lugha yenye mvuto, wahusika walioboreshwa na hali zinazozua kicheko.

Kauli ya mmoja wa watoa taarifa inabainisha kwamba:

*"Wanaonekana kuuvaa uhusika wa kike katika maigizo yao lakini katika mazingira yao ya kawaida huwakuti kuvaa uhusika huo… hivyo kuvaa kwao uhusika wa kike ni kusababisha hadhira ipate burudani".*

Chanzo: Data ya Uwandani (2025)

Kwa mujibu wa Wamitila (2002), komedia ni utanzu wa kidrama unaolenga zaidi kufurahisha hadhira, lakini pia hubeba maudhui ya kijamii. Katika komedia zilizoshughulikiwa na utafiti huu, ucheshi hutokana na matumizi ya sauti ya kike, mitindo ya mavazi, utendaji wa mwili na tabia zinazofanana na wanawake, ambavyo vyote kwa pamoja huchochea hisia za furaha kwa watazamaji.

Kwa kuhusisha na nadharia ya upokezi wa hadhira ya Hall (1973), uvaaji huu unasababu zilizofichwa nyuma yake kwa madhumuni tafauti. Katika muktadha wa komedia, madhumuni haya ni kuiburudisha hadhira, hivyo uvaaji wa uhusika wa kike ni sehemu ya matumizi ya mitindo ya lugha, vitendo na uwasilishaji unaolenga kufanikisha dhima hiyo.

Lihamba (2004) anaeleza kuwa kazi yoyote ya sanaa ina wajibu wa kuelimisha, kuburudisha na kuonya. Vivyo hivyo, waigizaji kama Joti na Pungasese wameweza kutumia kipengele hiki cha kuburudisha kupitia uvaaji wa uhusika wa kike kwa ufanisi mkubwa na hivyo kujenga mvuto wa kudumu kwa hadhira yao. Hali hii inaonesha kuwa burudani si lengo la juu juu pekee, bali pia ni nyenzo ya kufikisha ujumbe, kujenga uhusiano na jamii na kuendeleza sanaa yenye tija kijamii.

### 5.1.7 Uhuru wa Wasanii

Uhuru wa wasanii ni moja kati ya sababu kuu zinazowasukuma waigizaji wa kiume kuvaa uhusika wa kike katika komedia za Kiswahili. Utafiti huu umebaini kuwa wasanii wengi wanatumia fursa ya uhuru wa kisanaa kama jukwaa la kujaribu mitindo mipya ya uigizaji bila kujali mara zote athari zake kijamii na kiutamaduni.

Kwa mujibu wa mtoataarifa D:

*"Ingelifika mahali kwa matendo kama haya, baraza la sanaa wangeliamua uhusika wa kike waachiwe wanawake wenyewe, kwani ndipo watakapo uwakisi uhusika wao".*

Chanzo: Data ya Uwandani (2025)

Kauli hii inaonesha jinsi ambavyo uhuru wa kisanaa, ingawa ni haki ya msingi ya msanii, unaweza pia kuwa na athari kwa hadhira na jamii endapo hautasimamiwa ipasavyo. Hali hii imekuwa ikionekana zaidi katika tasnia ya komedia ambapo, kwa kisingizio cha uhuru wa kujieleza, wasanii huvaa uhusika wa jinsia tafauti, wakieleza au kuonesha mambo yanayoweza kuwa na athari kwa maadili ya kijamii.

Kwa kuzingatia msingi wa pili wa nadharia ya upokezi wa hadhira ya Hall (1973), katika muktadha wa komedia, uhuru huu hujidhihirisha kupitia matumizi ya lugha, mavazi na mienendo ya uigizaji

ambayo kwa baadhi ya watazamaji inaweza kuwa kinyume na maadili. Hali hii inasisitizwa na baadhi ya watoa taarifa waliodai:

"*Bodi ya sanaa ya Zanzibar inakagua kipengele kimoja kimoja… ila inaonekana huwenda baraza la sanaa Tanzania wamewapa uhuru wa kupitiliza wasanii wao".*

Chanzo: Data ya Uwandani (2025)

Hii inaonesha tafauti ya mitazamo ya taasisi za udhibiti wa sanaa kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, ambapo Zanzibar inaonekana kuwa makini zaidi katika kulinda maadili ya kijamii kupitia udhibiti wa sanaa. Mfano halisi ni kufungiwa kwa baadhi ya wasanii wanaotumia lugha za matusi au mavazi yasiyofaa kwenye nyimbo, huku wasanii wa maigizo wakionekana kuachwa huru zaidi licha ya maudhui yao kuwa na athari zinazofanana.

Wamitila (2002) anaeleza kuwa uhuru wa kisanaa ni nyenzo muhimu ya ubunifu, lakini unapaswa kusawazishwa na wajibu wa kijamii. Kwa hiyo, uvaaji wa uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume, licha ya kuwa ni ishara ya uhuru wao wa kisanaa, pia unaibua hoja ya kama uhuru huo unatumika kwa tija au unakiuka maadili ya kijamii.

Hivyo, utafiti huu unathibitisha kuwa uhuru wa wasanii ni mojawapo ya sababu kuu zinazochochea uvaaji wa uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume, ambapo uhuru huo huwasukuma kujaribu mbinu mpya za kisanaa bila kizuizi madhubuti kutoka kwa taasisi husika.

Kwa mujibu wa data zilizokusanywa kupitia usaili, utafiti huu umebaini kuwa sababu kuu zinazowasukuma waigizaji wa kiume kuvaa uhusika wa kike katika komedia za Kiswahili ni pamoja na kutafuta kipato, ubunifu, ubinafsi, uwezeshwaji, kutaka umaarufu, dhima ya kuburudisha na uhuru wa kisanaa. Sababu hizi zinaonesha kuwa uvaaji huo ni mkakati wa kisanaa unaotumika kufanikisha malengo ya kijamii, kiuchumi na kisanii wa waigizaji hao.

## 6.0 HITIMISHO

Utafiti huu umeangazia msukumo wa uvaaji wa uhusika wa kike kwa waigizaji wa kiume katika komedia za Kiswahili, kwa kutumia nadharia ya Upokezi wa Hadhira ambayo imesaidia kuchambua namna hadhira inavyopokea na kutafsiri kazi hizi za sanaa. Kwa mujibu wa data zilizokusanywa kupitia mbinu ya usaili, utafiti huu umebaini kuwa sababu kuu zinazowasukuma waigizaji wa kiume kuvaa uhusika wa kike katika komedia za Kiswahili ni pamoja na kutafuta kipato, ubunifu, ubinafsi, uwezeshwaji, kutaka umaarufu, dhima ya kuburudisha na uhuru wa kisanaa. Sababu hizi zinaonesha kuwa uvaaji huo ni mkakati wa kisanaa unaotumika kufanikisha malengo ya kijamii, kiuchumi na kisanii wa waigizaji hao. Hivyo, mtafiti anahitimisha kuwa, ipo haja kwa wasanii wa komedia kuzingatia maadili ya jamii, uhalisia wa jinsia wanazozimithilisha na hadhira wanayolenga, ili sanaa yao ibaki kuwa nyenzo ya kuelimisha, kuburudisha na kujenga jamii yenye maadili chanya**.**

## MAREJEO

Abrahams, R. D. (1992). *Singing the master: The emergence of African American culture in the plantation South*. Pantheon Books.

Albrecht, J. M. (2012). *Reconstructing individualism: A pragmatic tradition from Emerson*. Fordham University Press.

Bakhtin, M. M. (1984). *Rabelais and his world (H. Iswolsky, Trans).* Indiana University Press.

Butler, J. (1990). *Gender trouble: Feminism and the subversion of identity*. Routledge.

Decherney, P. (2011). Gag orders: Comedy, Chaplin and copyright. In Saint Amour (Ed.), Modernism and Copyright (pp. 163–164). https://www.quora.com

Frankelius, P. (2009). Questioning two myths in innovation literature. *Journal of High Technology Management Research*, 20(1), 40–51.

Hall, C. S. (1973). *Encoding and decoding in the television discourse*. University of Birmingham.

Hill, J. S. (1997). *The romantic imagination*. Macmillan Press Limited.

Jin, H. (2011). British culture studies, active audiences and the status of cultural theory: An interview with David Morley. Theory, Culture na Society, 28(4), 124–144.

Kennedy, X. J., & Gioia, D. (2007*). Literature: An introduction to fiction, poetry, drama and writing (10th ed.).* Longman.

Kothari, D. (1990). *Research methodology: Methods and techniques.* New Age International (P) Ltd.

Lihamba, A. (2004). *Politics and theatre in Tanzania after the Arusha Declaration 1967–1984.* Dares Salaam University Press.

Limbe, M. (2014*). Sanaa ya maonyesho*. Kenya Literature Bureau.

Lucas, C. B., & Seleman, M. (2022). Utendaji katika vichekesho vinavyowasilishwa kwa njia ya elektroniki: Uchunguzi wa vichekesho vya Ze Orijino Comedi. *Nuru ya Kiswahili*, 1(2), 212–235.

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za nathari ya Kiswahili: Tamthilia, riwaya na hadithi fupi.* East African Educational Publishers.

Moyles, D. (2002). *Observation and research tool.* In Research methods in educational leadership and management (pp. 172–195).

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili: Kozi za fasihi vyuoni na vyuo vikuu.* Moccony Printing Press.

Ndalu, A. E., Babusa, H., & Mirikau, S. A. (2014). *Kamusi teule ya Kiswahili: Kilele cha lugha*. East African Educational Publishers.

Njogu, K. (2010). Introduction to African oral literature and performance. Twaweza Communications.

Romos, M. D. M., Costa, A. B., & Cerqueira-Santos, E. (2020). Effeminacy and anti-effeminacy: Interactions with internalized homophobia, outness and masculinity. Trends in Psychology, 28 (3), 337–352.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa lugha na fasihi*, Kitabu cha Kwanza. KAUTTU.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili sanifu. (Toleo la 2).* Oxford University Press East Africa.

TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili sanifu (Toleo la 3).* Oxford University Press East Africa. Kamusi Elezo Huru. (2024). https://sw.m.wikipedia.org/wiki/Joti

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publishers Ltd.

Webster, J. G. (1998). The audience. *Journal of Broadcasting na Electronic Media*, 42(2), 190–
ya.com.